**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA MAAFISA BIASHARA WA MIKOA NA WAKUU WA IDARA ZA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI KATIKA HALMASHAURI ZA TANZANIA BARA UTAKAOFANYIKA TAREHE 06 APRILI, 2024 MKOANI MOROGORO**

- **Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara;**
- **Ndugu Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI;**
- **Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro;**
- **Mkuu wa Wilaya Morogoro;**
- **Ndugu Godfrey Simango Nyaisa, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA;**
- **Wakuu wa Taasisi mliopo;**
- **Wajumbe wa Menejimenti za Wizara na BRELA;**
- **Maafisa Biashara wa Mikoa;**
- **Wakuu wa Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu Kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**
Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa siku hii ya leo tukiwa na afya tele kwa ajili ya kushiriki mkutano huu muhimu baina ya Wizara pamoja na Maafisa Biashara wa Mikoa na Wakuu wa Idara za Biashara, Viwanda na Uwekezaji kwa lengo la kukaa pamoja na kujadili mustakabali wa kukumbushana wajibu wetu ili kuboresha zaidi utendaji wa majukumu yetu.

Pili, napenda kukushukuru **Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi** kwa kukubali kuacha majukumu yako na kuja kujumika nasi katika kikao hiki muhimu. Nakushukuru sana! Natambua kuwa wewe ndiyo msimamizi mkuu wa utekelezaji wa sera zinazosimamia sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji katika mikoa na Halimashauri zote nchini. Hivyo, kiufupi kikao hiki ni chetu sote kwani kitasaidia kuborehsa utendaji kazi kwa Maafisa hawa.

**Ndugu Washiriki;**
Kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Pia, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuridhia uanzishaji wa Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ni kwa muda mrefu suala hili limekuwa katika mchakato lakini ni katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, suala hili limepata jawabu na sasa kuna Idara katika Halmashauri zetu ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria Kanuni na Miongozo mbalimbali ya kusimamia masuala ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji katika Halmashauri na Mikoa yetu.

niwashukuru Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA na timu yake kwa kutuwezesha kukutana hapa katika mkutano huu. Natambua kwamba BRELA ikiwa ni Wakala ya Serikali iliyo chini ya Wizara yangu, ina mambo mengi ya kutekeleza lakini wameona umuhimu mkubwa wa kuwa na Mkutano huu kati yangu, Maafisa Biashara wa Mikoa yote na Wakuu wa Idara za Uwekezaji Viwanda na Biashara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara.

Niwashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri kutoka Mikoa yote Tanzania Bara kwa kuwaruhusu Maafisa Biashara Mikoa na Wakuu wa Idara za Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuja kushiriki katika Mkutano huu. Niwapongeze Maafisa Biashara wa Mikoa na Wakuu wa Idara mliopo hapa kwa fursa hii mliyoipata ya kuhudhuria mkutano huu muhimu. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza kwa kuaminiwa kuwa Wakuu wa Idara hii mpya ambayo ni muhimu sana katika ujenzi wa Mazingira wezeshi ya uwekezaji, uanzishaji na uendelezaji wa viwanda na biashara. Ni mategemeo yangu kuwa mkutano huu utakuwa ni nafasi nzuri ya kuelewa vizuri majukumu yenu na matarajio ya Serikali hususan Mh. Rais aliyeianzisha Idara hii.

Mwisho lakini si Kwa Umuhimu, Niwashukuru Waandishi wa Habari kwa kutenga muda na rasilimali zenu kuwepo hapa na kushiriki ufunguzi wa Mkutano huu, ni imani yangu kuwa taarifa za mkutano huu zitawafikia wananchi kwa haraka na katika njia mbalimbali ili wapate ufahamu wa uwepo wa Idara hii katika Halmashauri na waweze kuzitumia kwa huduma za urasimishaji wa Biashara viwanda na uwekezaji kwa ujumla.

**Ndugu Washiriki;**

Nimeona ni muhimu kuitisha Mkutano huu kati yangu na ninyi ili tuweze kujadili kwa pamoja majukumu tuliyonayo na kujipanga kwa ajili ya kufikia malengo na matarajio ya Serikali katika kuanzisha Idara hiyo.

Tunafahamu kwamba Idara hii imeanzishwa hivi karibu ili kutatua changamoto za kimuundo zilizosababisha kutokuwa na uratibu mzuri wa Masuala ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na kushindwa kuwatumia kikamilifu Maafisa Biashara katika shughuli za kisekta. Hali hii ilisababisha changamoto kwa Serikali kutofikia malengo yake, hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa shughuli za Wizara hufanyika katika ngazi za Mikoa na Halmashauri.

Ili kutatua changamoto hizo, Serikali iliandaa Muundo wa Mgawanyo wa Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wa tarehe 29 Januari 2022, ambao ulianzisha Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, baadae Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI tulitoa Mwongozo wa utekelezaji wa Muundo Mpya wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ukijumuisha uwepo wa Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji. Ni matumaini yangu kuwa, Mwongozo huo utatumika kama nyenzo muhimu ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini.

**Ndugu Washiriki;**

Wizara ya, Viwanda na Biashara inatekeleza majukumu yake ya kimuundo kwa kuzingatia Muundo wa Utumishi wa Umma wa mwaka 2022, maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali, sambamba na mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs 2030); Agenda ya Afrika 2063; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025; na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26. Ili kutekeleza majukumu hayo, Wizara inatumia nyenzo mbalimbali ikiwemo Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ili kusimamia sekta hizo.

Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imeendelea kuboresha mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara, uwekezaji na uendelezaji wa viwanda, kwa kuweka mifumo yenye tija ili kuchochea mageuzi ya sekta hizo na hatimaye kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa kutumia rasilimali zilizopo na kuzingatia umuhimu wa sekta katika kukuza uchumi na

kuongeza fursa za ajira. Baadhi ya mifumo hii ni pamoja na Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathimini, Mfumo wa Ukusanyaji Mapato, Mifumo ya sajili za kibiashara na ya Utoaji wa Leseni.

**Ndugu Washiriki;**

Muundo wa sasa uliopitishwa mwaka 2022 na Mwongozo uliotolewa umeainisha majukumu ya Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika kusimamia maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji kupitia Sera na Mikakati mbalimbali inayosimamia sekta hizo nchini. Ni matarajio yangu na Serikali kwa ujumla kuwa Mwongozo huu utaongeza ufanisi na kuleta ustawi wa sekta za viwanda, biashara na uwekezaji pamoja na kuchochea maendeleo ya ukuaji wa uchumi nchini.

**Ndugu Washiriki;**

Mwongozo huo una lengo la kujenga uelewa wa pamoja na misingi ya utekelezaji wa majukumu ya idara ya viwanda biashara na uwekezaji ili kuwa na mazingira bora na shindani ya uwekezaji na ukuaji shirikishi wa viwanda na biashara, kutafsiri kwa vitendo uwepo wa Idara hiyo katika Mikoa na Halmashauri zetu na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Watalaam wa Biashara wanaohudumia sekta ya viwanda na biashara kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Malengo mahususi ya Mwongozo huu ni pamoja na:-

i. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa masuala ya sekta ya viwanda na biashara katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri;
ii. Kuwezesha watendaji wa Serikali na wadau mbalimbali kuelewa majukumu na shughuli zinazotekelezwa kwenye Sehemu na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.
iii. Kuratibu upatikanaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa masuala yanayohusu sekta ya viwanda na biashara; na
iv. Kuongeza uwajibikaji na uwazi wa Wataalam wa Biashara katika kusimamia maendeleo ya sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji nchini.

**Ndugu Washiriki;**

Muundo huo pia umeainisha majukumu ya Wataalam wa Biashara katika Sehemu na Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kwa kuzingatia uwepo wa Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia masuala ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambaye anawajibika kwa Katibu Tawala Mkoa na

Mkuu wa Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji katika ngazi ya halmashauri ambaye anawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Katika Mkutano huu, tutapitia kwa pamoja majukumu ya sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Sekretarieti za Mikoa na majukumu ya Idara za Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Ndugu Washiriki;**
Nimewaiteni ninyi nikitambua kwamba ndiyo mlioaminiwa kuongoza sehemu na Idara za Viwanda Biashara na Uwekezaji katika Mamlaka zenu ili tuyatafsiri na kuyaelewa kwa pamoja majukumu mliyonayo, matarajio na matokeo tarajiwa ya uanzishwaji wa Sehemu na Idara hizo katika maeneo yenu. Kama ninyi viongozi msipo zielewa na kuzitafsiri ipasavyo itakuwa ni vigumu kwa Maafisa walio chini yenu kuweza kutafsiri na kuelewa majukumu yao na kuyatekeleza inavyopaswa.

**Ndugu Washiriki;**
Mwongozo umeweka utaratibu wa uratibu wa masuala ya Kisekta katika Ngazi zote za Serikali yaani ngazi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Ngazi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Ngazi za Mikoa na katika Ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa bila kusabisha mgongano wa maslahi au ya kiutendaji. Ni vema kila mhusika akafahamu majukumu na mipaka yake, mahusiano ya kiutendaji na kiwajibikaji katika uratibu na utekelezaji wa masuala ya kisekta.

Pia, Mwongozo huo umeweka mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini utakaotumika kufuatilia mwenendo na maendeleo ya utekelezaji wa mwongozo huu na matokeo au tija ya kuanzishwa kwa sehemu na Idara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji katika Mikoa na Halmashauri. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini unatumika sambamba na Mwongozo wa Maafisa Biashara katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wataalam wa Biashara. Hivyo basi, mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unashughulikia kazi zote zinazofanywa wakati au baada ya utekelezaji wa majukumu ya Idara katika kufafanua, kuchagua, kukusanya, kuchambua na kutumia tarifa za utekelezaji. Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini utatoa picha ya wazi ni nini kimetendeka, wapi pametekelezwa vizuri au vibaya na kutambua maeneo yanayohitaji uboreshaji, na kutoa mapendekezo kwa hatua za baadaye.

**Ndugu Washiriki;**
Kama mnavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania,

imedhamiria kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara nchini ili kuendana na azma ya kufanya mageuzi ya kiuchumi na viwanda kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu ya jamii, kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III).

Napende kuchukua nafasi pia kuwakumbusha kwamba dunia imeshaingia katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda (4th Industrial Revolution) ambayo yanajikita katika matumizi makubwa ya teknolojia yanayohusisha matumizi makubwa ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence), uharaka wa utoaji wa huduma, watu kukutana kidigitali na uwepo wa maarifa ya kutosha na yasiyo na mipaka kwa jamii kwa njia za kidigitali. Mapinduzi haya yanaenda kuongeza ushindani, kukuza uchumi kwa kasi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa njia za kidigitali.

**Ndugu Washiriki;**
Katika kufanikisha dhamira hiyo, na kuendana na Mapinduzi ya nne ya Viwanda, sehemu na Idara zilizoanzishwa katika Sekratarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinatakiwa kuchochea ukuaji wa sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji na kuboresha uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa mipango, mikakati na programu mbalimbali za kisekta. Je tumejipangaje?).

**Ndugu Washiriki;**
Nafahamu juhudi ambazo zimekuwa zilifanyika na Serikali hususani BRELA ya kutoa mafunzo kwa Maafisa Biashara kuhusu Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208, Sheria ya Taifa ya Usajili na Leseni za Viwanda Sura ya 46 na shughuli za Sajili mbalimbali zinazofanywa na BRELA. Nimetaarifiwa kwamba Tangu kuanza kutolewa kwa mafunzo haya mwaka wa fedha 2021/22, Maafisa Biashara 637 wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wamenufaika kutoka Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Ni matarajio ya yangu na Serikali kwa ujumla kwamba, Maafisa Biashara hao watatumia elimu hiyo, kufanya majukumu yenu ya msingi, ya kuwa wawezeshaji na washauri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, ili Sekta hii ikue kwa kasi inayoendana na Dira, Dhima na Mipango Mkakati ya Serikali.

Tusiendelee kufanya kazi kimazoea kutokana na kuwa mlikuwa chini ya Idara ya mapato ambako mlijikita kwa asilimia kubwa kuwa wakusanya mapato. Tunatakiwa tubadilike sasa na kuwa na mtizamo mpya wa kuwa marafiki na washauri wa wafanya biashara na kufanya majukumu yetu kwa weledi mkubwa. Wafanyabiashara wanapaswa kutuona kuwa ni marafiki na kutukimbilia  na sio maadui na kutukimbia

kwani tukiwa na mahusiano mazuri nao biashara zitakua na ndiyo kuongezeka kwa uchumi wao, mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali na hatimae kukua kwa uchumi wa Taifa kwa ujumla.

**Ndugu Washiriki;**
Wito wangu kwenu na kusudi la kuwaleta kwenye mkutano huu ni kupeana dondoo na uelewa wa majukumu ya Idara, namna shughuli za kisekta zitakavyoratibiwa, umuhimu wa utoaji wa taarifa pale zinapohitajika na kujipanga kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu katika kipindi ambapo dunia inabadilika kwa kasi sana, ushindani wa kibiashara na kiuchumi ni mkubwa, Dunia imekuwa kama kijiji

Utendaji kazi wetu mzuri na tija itakayo patikana ndiyo itakayo ithibitishia Serikali umuhimu wa kuanzisha Idara hii pamoja na umuhimu wa Kada ya Maafisa Biashara kwa ujumla katika Mikoa na Halmashauri zetu. Ni imani yangu kuwa mkitoka hapa mtaenda kuwa washauri wazuri wa wakuu wenu (Wakurugenzi, Makatibu Tawala na Wakuu wa Mikoa) kwa masuala ya sekta mnayo isimamia, mtaandaa mipango na mifumo mizuri ya utendaji kazi, mtaongeza ubunifu na uharaka wa kufanya maamuzi yenye tija kwa uwekezaji, viwanda na Biashara.

**Ndugu Washiriki;**
Nimelize hotuba yangu kwa kuwakaribisha sana hapa Morogoro na kuwaomba mtumie vema siku hizi mbili kwa ajili ya kujijengea uwezo, kubadilishana uzoefu na kukuza mtandao wa kimawasiliano miongoni mwenu ili pale mtu anapopata changamoto awasiliane na wenzake kwa ajili ya kujifunza na kupata uzoefu zaidi.

Niwashukuru tena BRELA kwa kuratibu mkutano huu na ni imani yangu kuwa washiriki hawa wataenda kuwa mabalozi wazuri na mfano bora kwa sehemu na Idara nyingine katika utoaji wa huduma bora na wezeshi zinazoendana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda katika uchumi wa Dunia.

**Ndugu Washiriki;**
Baada ya kusema haya, napenda kuchukua nafasi hii kutangaza rasmi kuwa Mkutano huu wa siku mbili wa Maafisa Biashara wa Mikoa na Wakuu wa Idara za Viwanda Biashara na Uwekezaji umefunguliwa Rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!**